## HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,
Halmashauri ya Wilaya,
**USHETU**

**TAARIFA YA ZIARA KUJIFUNZA UKUSANYAJI WA MAPATO HALMASHAURI YA SHINYANGA TAREHE 28/04/2022 – 29/04/2022**

### 01: UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**
Naomba kuwasilisha taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa kuzingatia agizo la Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 24 – 25/02/2022 ambapo iliagizwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kusimamia na kufuatilia ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kutoka kwenda maeneo mengine ya Halmashauri zinazofanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato kujifunza mbinu wanazotumia katika ukusanyaji mapato ikiwa ni pamoja na kufuatilia ramani iliyotumika kujenga soko la madini mwabomba kama ni sahihi na inafanana na ramani za maeneo mengine ya masoko ya madini.

Mnamo tarehe 28/04/2022 Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilifanya ziara Halmashauri ya Shinyanga kwenda kujifunza mbinu/ njia zinazotumika katika ukusanyaji wa mapato na kubaini mambo yafuatayo:-

**(a) Eneo la Madini /Uchimbaji wa dhahabu**

i) Kabla ya zoezi la uchimbaji wa madini kuanza kilifanyika kikao baina ya Halmashauri na wachimbaji na kukubaliana yafuatayo:-

**Wachimbaji**

- kulipia ushuru wa viroba , kila kiroba Sh. 1,000/=
- Ushuru wa karasha Sh.10,000/= kwa mwezi ambapo fedha ililipwa Sh.120,000/= kwa miezi 12 kwa kila karasha na fedha hiyo ilikusanywa kwa siku moja kwa kutumia *"team work"*
- Wanaotoa viroba vya mchanga nje ya mgodi wanalipia Sh. 2,000/= ambapo walikubaliana na Ofisi ya Madini kuhakikisha kibali wanachotoa ya kusafirisha viroba nje ya mgodi ni kuanzia mifuko 20,000 na kibali husika hutolewa na Katibu Mkuu Madini
- Kuhamisha senga /mchanga wa marudio kwenda kwenye plant kwa roli/ gari kila tripu Sh.50,000/=
- Magari yanayobeba mawe kupeleka kusaga kila tripu Sh. 10,000/=
- Kila anaye katiwa duara kwa ajili ya uchimbaji analipa Sh. 200,000/= kwa mwenye eneo na Halmashauri inachukua 10% katika fedha iliyolipwa
- kila tripu ya *"timber"* inalipiwa Sh. 30,000/=

ii) Soko la Madini

**Mhe. Mwenyekiti,**

Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango walifanikiwa kufika katika soko la madini eneo la Mwakitoryo Halmashauri ya Shinyanga ambapo soko hilo ni la mtu binafsi na makubaliano ya ujenzi yalifanyika kati ya "*blockers*" (Wauza Madini) na mwenye eneo.

Halmashauri katika eneo hilo inasimamia *"service levy*" na Ofisi ya madini inasimamia Mlahaba wa Serikali. Aidha, Halmashauri inachukua 0.3% ambayo ni "*service levy*" kutoka kwa "*blokers*", na imejiwekea mkakati kwa kushirikiana na Ofisi ya madini kuwa kutoa dhahabu kwenye eneo lao kwenda eneo lingine kunakuwa na kibali ambacho kinatolewa hivyo "*service levy*" italipwa eneo husika kilipotolewa kibali.

Katika soko la madini wakati wa uuzaji wa dhahabu kunakuwa na wasimamizi wanne ambao ni:-

i- Msimamizi kutoka Ofisi ya Usalama wa Taifa
ii- Msimamizi kutoka Halmashauri
iii- Msimamizi kutoka Ofisi ya Madini na
iv- Mnunuzi (Blocker)

ambapo kila mmoja wao atabaki na nakala ya mauziano kwa ajili ya rejea ya baadae wakati wa ufuatiliaji wa ushuru wa huduma.

**Kuhusu ramani iliyotumika katika ujenzi wa soko;-**

Eneo hilo halikufuata ramani kwa kuwa ni la mtu binafsi isipokuwa lilijengwa kwa kukidhi matakwa muhimu kama vile vyumba vya *blockers* na majiko yao ya kuchomea dhahabu, Ofisi ya Madini/Halmashauri na chumba cha Polisi.

iii) Mapato mengineyo

**Mhe. Mwenyekiti,**

Mapato mengineyo hukusanywa kupitia watumishi wa ngazi ya Kata ambao wao ni wasimamizi na wanalipwa 10% na fedha zinazokusanywa zinawekwa benki kwa kutengenezewa *"bill"* za malipo kila siku kwa wale ambao wapo mazingira ambayo hawawezi kuweka fedha kila siku wanapeleka benki kwa kila wiki, ambapo mwisho wa mwezi malipo ya 10% yanalipwa kwa kuangalia kilichokusanywa kwa mujibu wa Kata husika.

- Kuhusu ushuru wa mazao wanachaji kwa gunia Sh.2,000/= ambapo wanatumia ujazo wa kilo 100 kwa gunia na hakuna mzani wa kupima katika mageti
- Kwenye mageti kuna watu wameajiriwa kukusanya mapato na wataalam ngazi ya Kata ni wasimamizi
- Kuhusu makusanyo ya pamba suala hilo lipo chini ya bodi ya pamba wanaotoa vibali na Afisa Ushirika anafatilia takwimu Bodi ya pamba na inachajiwa 0.3% ya

bei iliyowekwa na Serikali. Aidha Bodi ya pamba inahusika kusimamia wale wenye madeni (makampuni) ambapo wanakuwa hawapewi leseni za ununuzi.

- Pumba za mpunga zinatozwa Sh .200/= ushuru wake na zao kubwa katika Halmashauri ni mpunga.
- Ushuru wa gulio unachajiwa Sh.500/= kwa kila mfanyabiashara kwenye gulio husika
- Kwenye minada mikubwa vyoo vimejengwa na wananchi wanalipia Sh.300/=
- Halmashauri imejiwekea utaratibu wa kukusanya na kudhibiti utoroshwaji wa mapato ambapo magari ya mizigo ya mazao/nafaka huruhusiwa kupita kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Hivyo yeyote atakayekiuka au kupita kinyume na muda tajwa hutozwa faini kwa mwenye mzigo na muhusika wa gari ambayo inaanzia Sh. 300,000/= na kuendelea.

***Uundaji wa taskforce / team work***

- Wataalam kutoka katika idara mbalimbali na Wakuu wa Idara wote ni sehemu ya timu hiyo ambapo kikosi kazi ambacho kipo mgodini kinalipwa Sh. 30,000/= kwa kila siku na wanaoenda katika ukusanyaji/doria wanalipwa Sh. 60,000/= kwa siku ikiwa ni pamoja na wanaoenda mnadani wanalipwa motisha Sh. 25,000/= kwa siku husika.

**MAONI YA JUMLA**

- Ufanyike uwezeshwaji wa magari na uwepo wa posho kwa timu ya ukusanyaji mapato
- Uwepo wa ukaguzi wa kushitukiza kwenye maeneo mbalimbali ya ukusanyaji mapato kwa kutumia *Task force/ team work*

**Maoni ya Wajumbe:** Wajumbe walipongeza kwa kazi nzuri inayofanyika ikiwa ni pamoja na mafunzo yaliyotolewa na mwenyekiti wa kikosi kazi.

Naomba kuwasilisha,

Theresia Nsumba

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

**Kny: Mkurugenzi Mtendaji**